# Procedure

## Investigating Reports of Sexual Harassment: Students INS-P032/Utaratibu wa uchunguzi wa unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi

Procedures are continually revised and improved. For the most recent version, please visit https://salkeiz.sharepoint.com/qam/SitePages/Home.aspx

1.0 **UPANA:**

1.1Utaratibu huu unaelezea mchakato wa kuripoti na kuchunguza unyanyasaji wa kinjinsia unaohusisha wanafunzi

2.0 **UTARATIBU:**

2.1 Msimamizi wa shule hupokea ripoti zote za unyanyasaji wa kijinsia unaohusisha wanafunzi

2.1.1 Wafanyakazi wote wa shule za Salem-Keizer huripoti wasiwasi wa unyanyasaji wa kinjisia unaohusisha mwanafunzi moja moja kwa msimamizi wa shule iwe kwa maneno au kwa maandishi

2.1.1.1 Ripoti inaweza kutokana na mfanyakazi kuona moja kwa moja au kupokea taarifa kutoka kwa mwanafunzi au mlezi au vyanzo vingine vya taarifa.

2.1.2 Wanafunzi wanahamasishwa kutoa taarifa ya unyanyasaji wa kijinsia kwa kufanya moja yafuatayo:

- Kamilisha ripoti ya siri iliyopo kwenye ofisi ya shule au ofisi za ushauri au
- Kutana na mkuu wa shule, msaidizi wa mkuu wa shule, mshauri, mshauri wa mambo ya tabia au mtu anayeaminiwa na shule au idara; au
- Toa taarifa kwa SafeOregon Tip line: Call or text 844-472-3367, email tip@safeoregon.com or visit www.safeoregon.com. Ripoti inaweza kuwa ya bila kujulikana

2.1.3 Mzazi/Mlezi au mwanajamii wanahimizwa kutoa taarifa kwa kukutana na msimamizi wa shule. Pia watu binafsi wanaweza kuripoti kama ilivyoonesha ADM-P008.

2.2 Mkuu wa shule anawajibu wa mwisho kuchunguza kila taarifa inayotolewa kuhusiana na unyanyasaji wakijinsia lakini pia anaweza kumchagua mtu au kuwashirikisha watu wengine kutokaofisizaSalemKeizerkuhakikisha hatua muhimu zinafuatwa.

2.2.1 Toa taarifa kwa afisa usalama wa shule au toa taarifa kwa vyombo vya sheria

2.2.2 Weka hatua za mpito kuhakikisha usalama wa mwanafunzi wakati uchunguzi unaendelea

2.2.3 Anzisha itifaki ya kujibu tukio la ngono (SIRC)Anzisha itifaki ya tishio kwa mwanafunzi (SIRC) au itifaki ya tathmini ya hatari ya kujiua (SRA)

2.2.4 Toa taarifa kwa mratibu wa safari za shule au meneja usafiri kwa ngazi ya wilaya/shule za Salem- Keizer kama kitendo kimetokea kwenye vyombo vya usafiri uliotolewa na Salem-Keizer au katika kituo rasmi cha basi.

2.2.5 Weka kumbukumbu juu ya malalamiko yote pamoja na nyaraka zilizoandikwa kuhusu uchunguzi

2.3 Uchunguzi lazima ujumuishe:

2.3.1 Hatua yeyote muhimu kuhakikisha kuwa mtu aliyeathiriwa analindwa na kukuza mazingira yasiyokuwa ya vitisho pamoja na:

- Kutoa nyenzo na hatua za msaada kwa mtu aliyeathiriwa; na
- Kuchukua hatua muhimu ili kuondoa athari inayoweza kutokea baadaye kwa mtu

aliyeathiriwa, ikizingatia kuwa hatua hiyo haiitalipiza kisasi dhidi ya mtu aliyeathiriwa au mfanyakazi yeyote aliyeripoti tabia hiyo kwa msimamizi wa shule

- Toa taarifa ya maandishi kama ilivyoainishwa

2.3.2 Mahojiano ya wanafunzi, watu wazima mwenye taarifa, mtu aliyeshuhudia au watu wengine ambao watachaguliwa na mkuu wa shule. Mahojiano yote yatafanywa binafsi na utambulisho wa mtu anayewasilisha ripoti hiyo itabaki kuwa siri kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria pamoja na sera ya utawala HUM A-029

2.3.3 Kupitia ushahidi wote uliopo.

2.4 Taarifa zinazohitajika kwa maandishi:

2.4.1 Ikiwa mwanafunzi, mfanyakazi au mtu mwingine atawasilisha malalamiko chini ya sera ya unyanyasaji wa kijinsia, msimamizi wa shule atatoa taarifa kwa watu wafuatao:

- Kila mtu anayeripoti
- Kama inafaa, mtu aliyeathirika ambaye siyo mtoa taarifa
- Kila mtu aliyetoa taarifa; na
- Pale inapowezekana mzazi au mlezi halali wa mtu anayeripoti, mtu aliyeathiriwa, au mtu aliyeripotiwa

2.4.2 Form INS-F082 Inatimiza mahitaji ya maandishi kama ilivyoanishwa katika sheria ya marekebisho (Oregon Revised Statute 342.704(4),) Kanuni za utawala (Oregon Administrative Rule 581-021-0038(5i)) na sera ya utawala (Administrative Policy HUM-A029.)

2.4.3 Mkuu wa shule atamjulisha kila mtu kama inavyoonesha kwenye 2.4.1 pale uchunguzi utakapo anza

2.4.4 Msimamizi wa shule atawataarifu kila mtu aliyeanishwa katika 2.4.1 uchunguzi utakopokamilika, na ikiwa ukiukaji wa sera uligundulika kutokea kufuata uchunguzi, kwa kiwango kinachoruhusiwa chini ya usiri wa mwanafunzi na sheria ya serikali

2.5 Katika hitimisho la uchunguzi, mkuu wa shule au yule aliyechaguliwa atachukua hatua kama inafaa, kushughulikia ukiukwaji wowote wa sera ya unyanyasaji wa kijinsia kwa lengo la kukomesha unyanyasaji, kuzuia usitokee na kuelezea matokeo na madhara yake.

3.0 **ASSOCIATED DOCUMENTS: Nyaraka husishwa**

HUM-A029, Sexual Harassment/**Unyanyasaji wa kijinsia**
PAP-A001, Child Abuse Reporting/**Kuripoti unyanyasaji wa watoto**
ADM-P008, Complaints, Public: Process for Resolving/**Malalamiko, umma: Mchakato wa kutatua**
INS-F030, Confidential Student Reports/**Ripoti za siri za wanafunzi**
INS-F082, Student-Guardian Sexual Harassment Notice: Impacted Person/**Taarifa kwa mwanafunzi/mlezi ya unyanyasaji wa kijinsia - aliyeathirika**
INS-F083, Student-Guardian Sexual Harassment Notice: Reported Person/Taarifa kwa MwanafunziMlezi unyanyasaji wa kijinsia - aliyeripoti

**4.0 REVISION HISTORY:**

| Date | Description |
|---|---|
| 6/3/19 | New procedure |
| 9/22/20 | Updates to comply with new legislation |

## 5.0 APPROVAL AUTHORITY:

5.1 Assistant Superintendent